

JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA



OFISI YA RAIS  
TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA  
HALMASHAURI YA MANISPAA YA Mtwara - MIKINDANI



Tarehe: 11/11/2021

### YAH: TANGAZO LA ZABUNI

Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara-Mikindani ni mojawapo ya Halmashauri zilizopokea Fedha zilizotokana na tozo ya miamala ya simu kwa ajili ya ujenzi wa kituo cha Afya Ufukoni( kupandisha hadhi zahanati ya ufukoni kuwa kituo cha Afya) awamu ya kwanza.

1. Mkurugenzi wa Halmashauri ya Manispaa ya Mtwara Mikindani anakaribisha maombi ya Mafundi wenyeji (local fundi), Taasisi za kiserikari au vikundi vya ujenzi wa majengo wenye sifa zifuatazo: -


- Awe na cheti cha ufundi kutoka chuo cha ufundi kinachotambulika na Serikali.
- Awe tayari kuheshimu mkataba wa kazi atakayopewa.
- Awe anajua kusoma michoro na ramani ya nyumba.
- Awe na uwezo, nguvu kazi ya kutosha, uzoefu wa kazi wa kujenga majengo ya serikali na vitendea kazi pamoja na kujenga, kumaliza na kukabidhi kwa Muda atakaopangiwa.
- Awe na Akaunti ya benki kwa ajili ya malipo ya kibenki kwa malipo ya kazi atakazokuwa anazifanya.



## ZINGATIO:

- Nguvu ya kisheria (Power of Attorney) ni kwa Taasisi za kiserikari au vikundi vilivyosajiliwa kisheria.
- Maombi yaambatanishwe na nakala ya vyeti vya ufundi na wasifu binasfi wa kazi
- Maombi yafungwe kwenye bahasha ya khaki (A4) yenye lakiri iandikwe kwa anuani ifuatayo:-  
Mkurugenzi wa Manispaa,  
Halmashauri ya Manispaa,  
S.L.P 92,  
**MTWARA-MIKINDANI.**
- Maombi yawasilishwe katika ofisi ya **MGANGA MFAUDHI**  
**ZAHANATI YA UFUKONI.**

Mwisho wa kupokea MAOMBI ni tarehe 19/11/2021 saa 5:00 asubuhi na ufunguzi utafanywa mara tu baada ya saa ya mwisho ya kupokea maombi na wawakilishi watakaoamua kuhudhuria ufunguzi huo wanakaribishwa.

  
COL. Emanuel H. Mwaigobeko  
**MKURUGENZI WA MANISPAA**

**MTWARA-MIKINDANI**

MKURUGENZI WA MANISPAA  
S. L. P. 92. MTWARA  
MIKINDANI